



HAKUNA UVUTAJI NDANI YA MAGARI YENYE WATOTO

Sheria Mpya inayozuia uvutaji kuanzia tarehe 22 Septemba 2010

Marufuku uvutaji ndani ya gari kipindi kuna mtoto ndani yake.

Uvutaji umepigwa marufuku ndani au kwenye magari hapa Western Australia kama umri wa mtoto ni chini ya miaka 17.

Mtu haruhusiwi kuvuta ndani au kwenye gari kama —

- gari lipo barabarani; na
- mtu mwengine yeyote aliyepo ndani au kwenye gari ni mtoto.

Mtoto

Inamaanisha ni mvulana au msichana ambaye hajafikisha umri wa miaka 17

Gari

Inamaanisha chombo chochote kinachoweza kutumika kusafirisha watu au bidhaa barabarani

Barabara

Inamaanisha barabara kubwa yeyote, barabara au mtaa uliowazi au njia inayotumiwa na umma na inajumuisha njia kubwa, njia za watembea kwa miguu, hifadhi, mahala pa kupishana na sehemu yeyote ya kuhifadhi magari.

Hatua za Kisheria

- Maofisa wa Polisi wa WA watakuwa na uwezo wa kutekeleza sheria hiyo, inayohusiana na uvutaji ndani ya gari kukiwa na watoto, kwa kushirikiana na Idara ya Afya.
- Maofisa wa Polisi wanauwezo wa kusimamisha gari na kuchukua taarifa za watu waliovunja sheria hizo mpya. Kisha watafikia taarifa hizo kwa Tawi linalohusiana na Udhambi wa Tumbaku waweze kufuatilia kuhakikisha hatua stahiki zimeshachukuliwa kama vile kutoa onyo, kutoa adhabu au kukufungulia mashtaka.

Ni muhimu kusisitiza kuwa sheria hii mpya inakubalika miongoni mwa jamii kwa kiwango kikubwa sana hivyo basi kutokana uzoefu wetu kutoka kwenye kipindi cha nyuma tunategemea kuwa wanajamii wa Western Australia watafuata na kutekeleza.

Adhabu

Kama kosa la uvutaji limefanyika ndani au kwenye gari pia kama kuna mtoto anaumri chini ya miaka 17 basi adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa kwa mtu aliyefanya kosa hilo:

- | | |
|---|--------|
| ■ Mahakama inaweza kukupa amri ya kulipa faini ya kiwango kisichozidi | \$1000 |
| ■ Unaweza kupewa Notisi ya Kulipa | \$200 |

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Tawi linalofuatilia Tumbaku:

Simu: 1300 784 892

Barua pepe/Email: tcb@health.wa.gov.au

Disclaimer:

The information contained in this factsheet has been produced as a guide only.

To view the full details in the relevant Tobacco Control legislation, visit www.health.wa.gov.au/tobaccocontrol

